# MAFANIKIO YA MITUME NO 1

<"xml encoding="UTF-8?>

BISMILAHI RAHMANI RAHIYMI

KWA JINA LA MWENYEEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU

MAFANIKIO YA MITUME

?Ni dalili gani zilizowasaidia Mitume kuweza kufikisha ujumbe wao kwa wanaadamu*

MAFANIKIO YA MITUME YA MWENYEEZI MUNGU NO.1

-:Mwenyeezi Mungu Mtukufu katika Qur-ani anasema hivi kuhusu Mitume

أُوْلَـئِكَ الَّذِينَ هَدَي اللّهُ فَبِهُدَاهُمُ اقْتَدِهْ قُل لاَّ اَسْاَلُكُمْ عَلَيْهِ اَجْراً إِنْ هُوَ إِلاَّ ذِكْرَي لِلْعَالَمِينَ[1]

Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu amewahidi. Basi fuata hidaya yao. Sema: Mimi sikuombeni .ujira. Haya hayakuwa ila ni mawaidha kwa walimwengu wote

Kwa hiyo kama tukifuata njia waliotuonesha Mitume, hapana shaka tutaongoka, basi ili kufuata njia hizo, ni lazima tuelewe siri ya mafanikio ya Mitume hiyo. Ama ni lazima tuzingatie kuwa tunaposema mafanikio ya Mitume haina maana kuwa watu wote wameongoka na kufuata njia -:ya Mitume, kwa sababu Mwenyeezi Mungu anasema

لَّسْتَ عَلَيْهِم بِمُصَيْطِرٍ[2]

.Wewe si mwenye kuwatawalia

Kwa hiyo tunaposema Mitume imefanikiwa katika kufikisha ujumbe wao, yaani Mitume imeweza kufikisha sauti ya Tawhiyd kwa wanaadamu wote ulimwenguni, na kuwataka watu wamuabudu Mola mmoja, Mola wa mbingu na ardhi. Kwa hiyo njia ya uongofu iko wazi kabisa kwa wale wacha Mungu, na kwa upande mwengine wameleta uadilifu, na kuwataka wanaadamu wawe waadilifu, na watake uadilifu, na kwa sababu hiyo basi nyoyo za wanaadamu ziliridhika na ujumbe wa Mitume hiyo, kiasi ya kwamba waliweza kuhifadhi imani yao kwa kustahamili tabu,mashaka, na adhabu walizokuwa wakizipata, watu hao walithibitisha ukweli wao, na walikuwa waaminifu katika kupigania haki ya kile walichokithibitisha na

kilichowathibitikia, wakapambanua baina ya haki na batili, na Mwenyeezi Mungu akawajaalia -:watu hao kuwa ni hoja kwa viumbe wake wengine, kama anavyosema ndani ya Qur-ani

رُّسُلاً مُّبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ لِئَلاَّ يَكُونَ لِلنَّاسِ عَلـَي اللهِ حُجَّةٌ بَعْدَ الرُّسُلِ وَكَانَ اللّهُ عَزِيزاً حَكِيماً[3]

Mitume hao ni wabashiri na waonyaji, ili watu wasiwe na hoja juu ya Mwenyezi Mungu baada .ya kuletewa Mitume. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima

Kwa hiyo, pindi wanaadamu wakifahamu sababu zilizowapelekea Mitume kufanikiwa katika kufikisha ujumbe wao, inaweza kutusaidia sisi katika kufuata njia zao. Basi katika makala ijayo .tutatupilia macho sababu muhimu za mafanikio ya Mitume

Surat Al _an-aam Aya ya 90 [1]

Surat Al-ghashiyah Aya ya 22 [2]

Suratun-Nisaa Aya ya 165 [3]

MWISHO